# Nishani ya Ndege

**Hatua ya 1**
**Kundi: Viumbe vya asili**
**Ilianzishwa mwaka 1928: General conference**

**1. Ndege nini/nani?**

Ndege ni kiumbe hai kama walivyo viumbe wengine walioumbwa na MWENYEZI MUNGU.

**2. SIFA ZA NDEGE**

Zipo sifa nyingi zinazofanya ndege watofautiane na viumbe wengine. Nazo ni hizi:

I. Wanaruka
II. Wana mayai yenye ganda gumu
III. Ni wenye damu joto
IV. Miili yao imefunikwa na manyoya
V. Mifupa yao ina tundu
VI. Bone structure in the eye
VII. Keen eyesight
VIII. Wana sauti nzuri za kimuziki.
IX. Ability to sense magnetic fields
X. Wana rangi nyingi zenye kupendeza

Pamoja na hayo wapo viumbe wengine pia wana damu moto, na wengine wana sauti kama vile chura. Hivyo hizo sifa hazifanyi ndege kuwa na utofauti na viumbe wengine. Aidha wengine wana uwezo mzuri wa kuona, na hivyo sifa hiyo haifanyi ndege kuwa tofauti.

**Kuna sifa maalum ambazo zinazofanya ndege kuwa tofauti kabisa na viumbe wengine. Nazo ni:**

i. Wanataga mayai yenye gamba gumu, ambayo huyaatamia na kuyatotoa kwa joto la mwili
ii. Miili yao imefunikwa na manyoya
iii. Mifupa yao ina uwazi inayowawezesha kuruka pasipo kutumia nguvu kubwa
iv. Wana mifupa wa duara katika macho yao ambao huwawezesha kulenga vema na hivyo kuwa na uoni makini.

**Kwa ujumla sifa/tabia zingine za ndege ni**

- Wana mabawa
- Wanaruka ingawa wengine hawawezi kuruka
- Wanataga mayai
- Wana vidole vitatu hadi vinne
- Miguu yao ina gamba ambalo huawezesha kutua au kupita mahapi popote
- Wana midomo kulingana na aina ya chakula wanachokula
- Wanaishi majumbani, porini na kwenye mapango.

## 3. Aina za ndege

Kuna makundi mbalimbali ya ndege kama ifuatavyo;

i. Ndege wanaofugwa: kuku, njiwa, khanga, bata, kuku mzinga n.k
ii. Ndege wanaoishi porini/majini; penguine, bata maji, mwewe, fundi chuma, Yangeyange, tai, kware, shomoro, furukombe n.k
iii. Ndege wanaoruka: Kweleakwelea,
iv. Ndege wasioruka: penguine, mbuni n.k
v. Ndege wanaokula nyama: Mwewe, kunguru, tai, fundi chuma n.k
vi. Ndege wanaokula nafaka: Shomoro, njiwa, kasuku, mbuni n.k
vii. Ndege wanaoruhusiwa kwa chakula, na wasioruhusiwa Mambo ya Walawi 11.

**Zingatia**: Chakula kikuu cha ndege ni nafaka, nyama, wadudu, majani n.k.
Baadhi ya ndege wasioruka ni;



**Cassowary**: Wanapatikana kwenye misitu ya kitropiki ya New Guinea na Kaskazini mashariki mwa Australia. Wanapenda kula vyura, konokono, wadudu na matunda yaliyo kwenye matawi ya miti mifupi, nyoka na wanyama wadogowadogo



**Kiwi:** Wanapatikana New Zealand. Chakula chao ni aina mbalimbali zaminyoo, mbegu, matunda, samaki wadogowadogo, na kwa kuwa wana midomo mirefu iliyochongoka huwasaidia kuwinda kwa urahisi



**Emu:** Ni ndege wakubwa kabisa anayepatikana Australia. Wanakula aina mbalimbali za mimea. Aina za mimea wanayokula hutegemea na upatikanaji wake kulingana msimu husika. Pia hula wadudu kama panzi, inzi n.k



**Rhea:** Wanapatikana Amerika ya Kusini. Ni ndege wanaokula vyakula vya aina zote nyama na mimea. Wanakula mbegu, mizizi, matunda, wadudu, mijusi, samaki na ndege.



**Penguin:** Ni ndege wanaoishi majini wanapatikana Hemisphere Kusini. Penguin wengi hula samaki, na aina mbali mbali za viumbe waishio majini, ambao huwakamata wanapoogelea chini/ndani ya maji. Nusu ya muda wa maisha yao huutumia nchi kavu na nusu nyingine baharini



**Ostrich:** Ni ndege wakubwa sana wanaoishi ukanda wa savanna katika Afrika.Wanakula mbegu/nafaka na aina mbalimbali za mimea, pia hula wadudu na mapanzi wakubwa. Hawana meno hivyo huweza kumeza mawe laini kuweza kusaidia kusaga chakula walichomeza. Mbuni wakubwa wanauwezo wa kubeba mawe yenye uzito wa kg 1katika tumbo lake. Ni ndege anayekimbia kuliko ndege mwingine yeyote duniani. Ana uwezo wa kukimbia kilometa 70 kwa saa. Pia ni ndege anayetaga mayai makubwa.

**4. a. Uumbaji wa ndege.**

Ndege ni viumbe walioumbwa siku ya tano katika juma la uumbaji.
Mwanzo 1: 20 – 23.

**b**. Biblia inayo majina mengi sana ya aina tofautitofauti za ndege. Baadhi yao ni kama ilivyoorodheshwa hapa chini. Ni vizuri kuyakariri majina na mafungu hayo.

- Kaati (Pelican), kunguru (Raven), bundi (Owl) - Isaya 34:11
- Kuku (Chicken) - Mathayo 23:37, Luka 13:34
- Tai (Eagle) – Yeremia 49:22, Yeremia 4:13, Ayubu 9:26, Kumbukumbu la Torati 28:49, Ayubu 39:27-29
- Mbuni (Ostrich) - Mika 1:8
- Njiwa (Dove) - Genesis 8:8-11, Matthew 10:16, Hosea 7:11
- Tai, furukombe, bundi, bundi mkubwa, mwewe, kipanga, kipungu, kiruka njia n.k Mambo ya Walawi 11:13-19
- Tausi (Peacock) - 1 Wafalme 10:22
- Kunguru - 1 Wafalme 17:6
- Kware (Partridge) - Yeremia 17:11

**5.** a. **Mambo muhimu ambayo katika hayo tunajifunza Upendo wa MUNGU uliooneshwa na makusudi yake katika umbaji wa ndege.**

"Children should be encouraged to search out in nature the objects that illustrate Bible teachings, and to trace in the Bible the similitude drawn from nature. They should search out, both in nature and in Holy Writ, every object representing Christ, and those also that He employed in illustrating truth. Thus may they learn to see Him in tree and vine, in lily and rose, in sun and star. They may learn to hear His voice in the song of birds, in the sighing of the trees, in the rolling thunder, and in the music of the sea. And every object in nature will repeat to them His precious lessons." Child Guidance, p. 46.

i. MUNGU aliumba ndege kuonesha kwamba Yeye mwenyewe ni mpaji wa kila kitu tunachohitaji. Ikiwa anawajali ndege, hakika Atatujali katika mahitaji yetu. Luka 12:24.
ii. Ndege hutufundisha juu ya MUNGU. Ayubu 12:7-9.
iii. Tunajifunza kwamba MUNGU anasema atatulinda kama vile kuku anavyolinda vifaranga wake. Mathayo 23:37.

iv. YESU alisema kwamba, MUNGU anaona shomoro anapoanguka, zaidi sana Anatuona sisi. Mathayo 10:29-31
v. Kwamba MUNGU atatupatia nguvu kama za tai. Isaya 40:31
vi. MUNGU ana uwezo wa kuwatumia ndege kutuhudumia. Mwanzo 8:6–12, Wafalme 17:6
vii. Ndege hutufundisha kwamba ni ishara ya ROHO MTAKATIFU. Mathayo 3:16

b. Uumbaji wa vimbe hawa unaonesha nguvu ya MUNGU ubunifu/usanii kwamba ni wa kiwango cha juu sana. Hebu tazama miguu, mkia na mabawa yanavyodhihirisha hilo.

c. Tunatakiwa kumwamini MUNGU kabisakabisa kama vile ndege wanavyofanya. Mathayo 6:26

d. YESU anampenda kila mmoja na kila kitu, tena anawajali sana wanyama kabla hajafanya lolote. Anatuhitaji tuwajali pia. Yona 4:11

Tusiwapige, tuwahurumie, tuwalishe na kuwalinda dhidi ya maadui.

**6.a. Faida za ndege**

i. Ndege hutumika kama chakula. Hutupatia mayai na nyama
ii. Husaidia kuingiza mapato (Biashara)
iii. Manyoya yake htumika kutengeneza nguo na mapambo
iv. Husaidia katika uzalishaji wa mimea, kwa kuchukua mbegu kutoka mahali fulani kupeleka katika mmea mwingine. Pia husaidia kusambaza mbegu
v. Hutupatia mbolea
vi. Husaidia kupunguza wadudu wakati wa ustawishaji wa mazao
vii. Husaidia kupunguza wanyama waharibifu wa mazao kama panya, sungura, n.k.
viii. Hutumika kama njia ya mawasilano. Mfano njiwa, kasuku
ix. Hutumika kama mapambona kupendezesha mazingira
x. Husaidia katika kutengeneza muziki
xi. Husaidia kusafisha mazingira. Mfano ndege wanaokula mizoga.
xii. Hutoa tahadhari ikiwa wameona kitu kibaya. Kuku, khanga, njiwa n.k

**b. Hasara za ndege**

i. Ni wachafuzi wa mazingira.
ii. Ni waharibifu wa mazao
iii. Huleta vijidudu vya maradhi kama mafua ya ndege, viroboto, utitiri n.k
iv. Ni wakorofi huweza kuuma anu kunyang'anya vitu. Mfano Kunguru
v. Wanapiga kelele mfano khanga.
vi. Wanahitaji uangalizi maalumu
vii. Wanakula sana. Wana tabia ya kuingiza na kutoa.

**7. Zingatia**

a. Tumjifunze MUNGU kwa kuangalia tabia za ndege
b. Kuwatunza kwa kuwapa huduma ndege kwa faida yako
c. Kutokuwa wakorofi kutowapiga wala kuwaonea bila sababu.
d. Tuwafundishe wawe rafiki zetu

**8. Fanya yafuatayo**

a. Tembelea moja ya bustani za wanyama au ndege na utambue aina tofautitofauti za ndege
b. Andika aina 10 za ndege wanaopatikana katika maeneo yako
c. Andika aina 10 za ndege kwa lugha ya kwenu
d. Tembelea msitu usio na wanyama wakali tambua viota vya ndege wanaopatikana katika eneo lako.
e. Andaa mazingira mazuri ya kufuga ndege.

**Tambua:** Mbuni ni ndege mkubwa kuliko wote na ni ndege anayekimbia kuliko wote na ana nguvu. Tai ni ndege mwenye nguvu, anaruka umbali wa km 120 kwa saa, sawa na km 50 kwa saa akiwa ardhini. Na anaona akiwa umbali mrefu sana. Ndiye ndegee pekee anayewafundisha watoto wake kuruka akiwa hewani kwa kuwabeba kwenye mbawa zake.

**MWISHO.**